**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 26/11/2021 KUJADILI TAARIFA YA FEDHA YA MWEZI OKTOBA**

**MAHUDHURIO:**

**Wajumbe:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Desderius O.Haule | Mwenyekiti | |
| 2. Ndugu Juma H. Juma | Mkurugenzi Mtendaji | Katibu |
| 3. Mh. Bahati G. Mbele | Makamu Mwenyekiti | |
| 4. Mh. Bosco Kapela | Mjumbe | |
| 5. Mh. Evelin Mwitumba | Mjumbe | |
| 6. Mh. Bosco Ndimbo | Mjumbe | |
| 7. Mh. Upendo Komba | Mjumbe | |
| 8. Mh. Gaudensia Kapinga | Mjumbe | |
| 9. Mh. Rehema Ndunguru | Mjumbe | |
| 10. Mh. Aron Hyera | Mjumbe | |
| 11. Mh. Bruno Kapinga | Mjumbe | |

**Wasiohudhuria:**

1. Mh. Benaya L.Kapinga (Mbunge) Mjumbe – kwa taarifa

**WATAALAM**

| | |
|---|---|
| 1. Ndugu Mfaume Cassim | Mkuu wa Idara ya Utumishi |
| 2. Ndugu Paschal Ndunguru | Mkuu wa idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 3. Ndugu Andrew Mbunda | Mkuu Wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 4. Ndugu Hillary Joseph | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 5. Eng. Neema Mbilinyi | Kaimu mkuu wa idara ya Ujenzi |
| 6. Dr. Louis Chomboko | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 7. Ndugu Cecilia Sasingwa | Afisa Utumishi |
| 8. Dr. Patrick P.Banzi | Mkuu wa Idara ya Mifugo |
| 9. Ndugu Jobu Mwalukosya | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 10. Ndugu Asante Luambano | Mratibu wa TASAF |
| 11. Ndugu Christoper Ntandu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 12. Ndungu Samwel Komba | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 13. Ndugu Sosteness Nakamo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira |
| 14. Eng. Evance Haule | Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika |
| 15. Ndugu John Kabada | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 16. Ndugu Salum Said | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Nyuki |
| 18. Ndugu Tumaini Mbunda | Mthibiti Ubora wa Shule |
| 17. Ndugu Maurus B. Hyera | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 18. Ndugu Samwel Marwa | Kaimu Mweka Hazina |
| 19. Ndugu Venant Kumburu | Afisa Utumishi |

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari
4. Yatokanayo na muhtasari huo
5. Taarifa ya Fedha ya Mwezi Oktoba 2021
6. Taarifa ya Fedha za Mikopo ya Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu
7. Taarifa ya Madeni ya Halmashauri
8. Mapokezi ya fedha za mradi wa kovid 19
9. Mapendekezo ya watia saini katika Akaunti ya Benki Kuu
10. Mengineyo
11. Kufunga kikao

**MDC/FUM/36/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:43 Asubuhi kwa kuwasalimia wajumbe na kumshukuru mwenyezi Mungu.

**MDC/ FUM /37/2021-2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilisomwa na kupokelewa na wajumbe.

**MDC/ FUM /38/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI**

Muhutasari wa tarehe 31.10.2021 ulipitiwa na wajumbe. Baada ya mapitio muhtasari ulisainiwa na katibu na mwenyekiti na kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**MDC/ FUM /39/2021-2022:YATOKANAYO NA MUHTASARI HUO**

**Mashine ya kukata vyuma ambayo ipo Tank la Maji Mbinga Mjini ifuatiliwe na kutolewa taarifa kwenye kikao kijacho.** Mashine hiyo ilifuatiliwa na kubaini ni mali ya Halmashauri na kwa sasa ipo Kata ya Mapera.

**Manunuzi yanayohusu ujenzi wa Boma yawe tofauti na manunuzi ya miradi mingine.** Agizo lilizingatiwa utekelezaji utaanza katika taarifa ya Robo ya Pili.

**Wadaiwa kwenye POS wakatwe posho zao za 10% ili wapunguze madeni yao.** Taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye kikao.

**MDC/ FUM /40/2021-2022 :MAPOKEZI YA FEDHA ZA MRADI WA KOVID 19**

Taarifa za mapokezi ya fedha zenye jumla ya Bil. 1.76 ziliwasilishwa kwenye kikao kwa ufafanuzi kwamba ni za ujenzi wa madarasa ya Sekondari yenye jumla ya madarasa 88. Aidha ilihimizwa fedha hizo zitumike kwa umakini ili zikamilishe kazi zilizokusudiwa.

Mwenyekiti alisema wahusika wote katika usimamizi wa kazi hiyo wajipange ili kutekeleza ili kuunga mkono jitihada za Serikali.

Wajumbe walikubaliana kusimamia kwa ushirikiano kati ya wataalam na waheshimiwa Madiwani.

Pia Bruno Kapinga aliunga mkono suala la ulipaji madeni ya wazabuni kutoathiri shughuli za uendeshaji wa Halmashauri.
Akihitimisha Mwenyekiti alisema watabariki ili madeni yaendelee kulipwa mara baada ya kuwasilishwa kwa mapitio ya bajeti yatakayofanyika mwezi Disemba 2021.

**MDC/FUM /43/2021-2022:MAPENDEKEZO YA WATIA SAINI KATIKA AKAUNTI YA BENKI KUU**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha mapendekezo ya watia saini hao katika kundi 'A' na 'B' kwa kuwataja wahusika hao kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini :-

| Jina la Akaunti | Watia Saini | | |
|---|---|---|---|
| BENKI KUU TANZANIA (BOT) | Group | A: | 1. Juma Haji Juma-Mkurugenzi Mtendaji<br>2. Samwel James Marwa-Kaimu Mweka Hazina |
| | Group | B: | 1.Mfaume Cassim Mfaume-Mkuu wa Idara ya Utumishi<br>2. Patrick Pius Banzi-Mkuu wa Idara ya Mifugo |

Wajumbe walipokea mapendekezo hayo na kuhimiza zoezi hilo lifanyike kwa uharaka ili kuendana na wakati.

**MDC/FUM /44/2021-2022 :MENGINEYO**

Mheshimiwa Bosco Ndimbo alipenda kujua kuhusu manunuzi ya vishikwambi kwa ajili ya matumizi ya waheshimiwa madiwani.
Akifafanua Katibu alisema taratibu za manunuzi ya vishikwambi zinaendelea.
Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuanzia Jumatatu tarehe 29.11.2021 ataanza ziara maalum ya kutembelea miradi ya **UVIKO** kwa lengo la kukagua utekelezaji wake.

**MDC/FUM /45/2021-2022:KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga M/kiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuhimiza ushirikiano kati ya Waheshimiwa na wataalam na hasa kwa suala la usimamizi wa miradi ya UVIKO . Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 6:16 mchana.

**= U M E T H I B I T I S H W A =**

**MWENYEKITI :**..[signature]....... **KATIBU :**..[signature]..........

**TAREHE :** 24.12.2021